**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule : 0755379021/0629367196**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0752360433**

**Matron/Patron : 0672437925/0717411041**

**Shule ya Sekondari : KIFARU**

**S.L.P :163**

**Tarehe 01/07/2024.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIFARU HALMASHAURI YA MWANGA MKOA KILIMANJARO MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Kifaru ipo umbali wa Kilometa 1.5 Kusini mwa Mji wa Kifaru. Usafiri wa pikipiki unapatikana kutoka kifaru standi hadi shuleni kwa nauli ya Shilingi 1000.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01 / 07 /2024 , hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30/06/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………..

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni oliver green sare 2. Kwa Wasichana na Oliver sare 2 kwa Wavulana. Maelezo ya mshono Wasichana sketi rinda box isiwe ya kubana na ndefu (inch 13 kutoka kwanye goti) wavulana iwe na marinda mawili mbele na chini isipungue upana inchi 17 (*kiambatanisho cha kitambaa cha sare ni hiki-oliver green);*



ii. Mashati 2 meupe mkono mifupi
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni bukta 01 na tsheti 01 ya dark blue isiyo na maandishi na track suti 1 ya dark blue Kwa wasichana na wavulana.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe (stocking) kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
viii. Sweta la oliver green(rangi ya sare ya shule)

ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) sketi nyeusi 2 kwa wasichana na suruali nyeusi 2 kwa wavulana (mshono uwe sawa na sare ya shule

x. Tisheti (T-shirt) moja dark blue yenye kola.



DARK BLUE

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 08 kubwa.
ii. **Ream (A4)** mbili ya karatasi kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
   - Cofa/mkebe (Mathematical Instruments set).
   - Four figure table (Logarithm table) kwa wanaosoma hesabu.
   - English dictionary (Kamusi ya Kiingereza ) na vitabu vingine vya kiingereza (kwa wanaosoma kiingereza).
   - Kamusi ya Kiswahili na vitabu vya Kiswahili (kwa wanaosoma Kiswahili)
   - Vitabu vya Geography (kwa wanaosoma Geography)
   - Vitabu vya History (kwa wanaosoma History)
   - Vitabu vya Economics (kwa wanaosoma Economics)
   - Vitabu vya Bam (kwa wanaosoma Bam)
   - Vitabu vya Advanced mathematics (kwa wanasoma EGM)
   - Calculator (Non programmable)
iv. Aje na godoro lake la futi 2.5
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya kijani mgomba, blanket 1 rangi ya kijivu, foronya ya godoro 1, chandarua 1
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (Kontena, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, Panga, jembe 1, mifagio 2 wa ndani na nje.mopper 01 ya kudekia.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Account namba ya shule 40201100020**
**NMB BANK.**
**NB: MZAZI UNAPO FANYA MALIPO ANDIKA MAJINA MATATU YA MWANAFUNZI KWENYE BANK SLIP.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni hakuna mwanafunzi yeyote anaye ruhusiwa kusuka.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS

KIFARU SECONDARY SCHOOL.
P. O. BOX 163,
MWANGA.

DATE:…………………

REF: NO. KHS/MEX/VOL.II/2023

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.

TO THE MEDICAL OFFICER,
………………………………………..
……………………………………….
……………………………………….

Please examine …………………………………… (Name of students) who has been selected to join this school for his fitness as a student in the following (To be completed by a medical officer)

1. Eye sight …………………………..
2. Hearing…………………………….
3. Limbs………………………………
4. SPECIMEN
   i) Stool………………….
   ii) Urine…………………
   iii) Blood…………………
   iv) Neurosis………………..
5. Asthma……………………………..
6. Tuberculosis ………………………
7. Pregnancy …………………………
8. Other serious disease:-
   i) Venereal disease……………………..
   ii) Leprosy …………………………..
   iii) Epilepsy ……………………………..
   iv) Ulcers …………………………………
   v)Sickle cell………………………………

MEDICAL CERTIFICATE:
(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above and consider him/ her to be physically fit / unfit as a student .
Date: ……………………………. Signature: …………………………………
Station : …………………………….   Designation:……………………………….
NB: I request this form to be returned to the school in a sealed – envelop.

**………………………….**
**THE HEADMASTER**

## *FOMU YA MAPOKEZI SHULENI*
## *MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI ( IRUDISHWE SHULENI)*

SEHEMU: "A" – Ijazwe na mwanafunzi;
Jina la Mwanafunzi ( majina matatu)

……………………………………………………………………………………

Anwani; ………………………………………………………………..

Taifa / Uraia : ………………………………………………………..

Dini : ………………………………………………………………………..
Tarehe ya kuzaliwa :…………………………… Jinsia :………………..
Shule anakotoka (Shule ya Sekondari ) :…………… ………………..Kata ya …………
Mwaka wa kumaliza kidato cha nne : ………………………………………………..
Wilaya anakotoka :……………………………………………………………….
Mkoa :…………………………………………………………………………..

SEHEMU "B" ( Ijazwe na mzazi/ mlezi)

Jina la mzazi / mlezi (majina matatu)

……………………………………………………………………………………..

Anwani ya mzazi/ mlezi :……………………………………………………….
Namba ya simu ya simu ya mzazi / mlezi……………………………………
Mahali anapoishi : ……………………………………………………………
Kazi ya mzazi / mlezi……………………………………………………………..
Mahali anapofanya kazi : ……………………………………………………….

SEHEMU "C"

a) Tafadhali fika na vifaa vyote ulivyoagizwa
b) Wahi shuleni kabla ya saa 11:00 jioni
c) Mzazi hakikisha unakamilisha malipo yote kabla ya kumleta mwanao shuleni .

………………………………..
SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI

……………………….
SAHIHI MKUU WA SHULE

FOMU YA MKATABA WA KUTOKUSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi ……………………………………………………………………..

Kidato cha :……………………….….. Mwaka:……………………..

Nakubaliana na maagizo yaliyoainishwa kwenye mkataba huu ya kutoshiriki kwenye migomo , fujo na makosa ya jinai kwa namna yoyote ile .

…………………………………… ………………
JINA LA MWANAFUNZI SAHIHI

TAREHE :…………………………..

…………………………………… …………........
JINA LA MZAZI / MLEZI SAHIHI

TAREHE:……………………………..

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Shule ya Sekondari Kifaru,

S. L. P. 163,

MWANGA.

Tarehe:……………….

## v. HATI YA UTII NA SHERIA

Mimi ……………………………………….. Mzazi / Mlezi wa ………………………………….. nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa katika Maagizo kwa Wazazi na nazikubali Sheria hizo na nitashirikiana na Shule kuona kuwa mwanangu anazizingatia kwa manufaa ya Umma.

Mimi ………………………………………………(majina matatu ya mwanafunzi)

Nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa na ninazikubali Sheria hizo. Naahidi kuwa nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa naelimishwa na Umma kwa manufaa ya Umma.

…………… .....                                        ……………........

SAINI YA MWANAFUNZI                                        SAINI YA MZAZI

TAREHE:………………

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………..**

**Jina la Mkuu wa Shule ABDALLAH .S. MOMBOKA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0755379021 /0629367196**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0752360433**
- **Mwandamizi Taaluma 0621511930**
- **Mwandamizi Malezi 0754072093**